

KANISA LA WAADVENTISTA WA SABATO UNIONI YA KUSINI MWA TANZANIA

CHAMA CHA WACHUNGAJI/HUDUMA ZA MAOMBI

SIKU 100 ZA MAOMBI: MACHI 27 – JULAI 04, 2020

MADA: KUMWITA YESU KATIKA HITAJI LETU LA HARAKA

Limeandaliwa na: Sikhu Daco – Mhariri Msaidizi wa Miongozo ya Shule ya Sabato - GC

Mtafsiri: Mch. Herbert I. Nziku – Mratibu - Huduma za Maombi: STUM

Juma la Kumi na Mbili, Juni 12 – Juni 18, 2020

WAKATI WA KUACHA HOFU NA KUTUMAINI TU

Mtoto wangu wa kwanza alipozaliwa, nilisoma kila kitu macho yangu yalichokiona kuhusu kila jambo ambalo lingeweza kwenda vibaya ndani ya siku chache za kwanza za maisha yake. Hata hivyo, wanasema, “kuonywa mapema ni kujizatiti mapema,” sawa? Alikuwa ni mtoto mwenye afya kamili, ametimia muda, akiwa na vidole vya mikono na miguu kumi, na vipimo vyote vya awali vilionesha matokeo kuwa bora kabisa. Lakini, nilipokuwa nautazama uso wake usio na hatia, ghafla nilishtushwa na ufahamu usio na mashaka kuhusu udhaifu wa uzima.

Nilipokuwa naendelea kusoma kwa kina, nilielekezwa juu ya SIDS (Sudden Infant Death Syndrome), yaani Dalili za Kifo cha Ghafla cha Mtoto Mchanga, na nilianza kuchunguza kwenye tovuti mbali mbali kwenye mtandao. Kila makala niliyoisoma, kila kisa cha mtu aliyepoteza mtoto kwa SIDS, viliniongezea tu wasi wasi kuhusu namna nisivyoweza kumlinda huyu mtoto wangu. Wakati fulani nilikuwa nasoma makala inayoshauri kutoweka kitu cho chote kwenye ubavu wa mtoto – si blanketi, wala mdoli wa mnyama – kwani kila kitu kinaweza kusababisha SIDS: Muda huo huo nilikutana na ushuhuda wa mama ambaye alifuata ushauri wote uliotolewa ili kumkinga mtoto dhidi ya SIDS, lakini asubuhi moja aliamka akikuta mtoto wake akiwa amekufa.

Vipi yule angekuwa ndio mtoto wangu? Ningefanya nini kuhakikisha kuwa famili yangu haikutani na mkasa kama huo? Nilikuwa nachoka kulala kwani nilikuwa naamshwa kila mara na kila mtikisiko, kila anapokohoa, na kila mabadiliko ya upumuaji wa mtoto wangu. Kama mke mwenye upendo, mwenye kuiamini kauli mbiu isemayo, “Kushirikisha ni Kujali,” nilimshirikisha mume wangu wasi wasi wangu, na siku ya kwanza ambayo mtoto wetu huyo wa kiume alilala zaidi ya saa sita, mume wangu alimwamsha ili tu kuhakikisha iwapo alikuwa bado anapumua. Unapata picha – tulikuwa na wasiwasi mkubwa mno!

Kwa kadiri nilivyo wazia namna nisivyo na uwezo wa kumlinda mtoto wangu dhidi ya SIDS, ndivyo ilivyokuwa wazi kwangu, namna juhudi zangu zilivyo dhaifu katika kuhakikisha usalama na kumlinda mtoto wangu. Kwa kweli, sikuweza kujihakikishia hata ustawi wangu mwenyewe, vipi kuhusu kitoto kisicho na uwezo!

Nikiwa nimezidiwa na hisia yangu ya kushindwa, nilimgeukia mama yangu, ambaye yeye alinigeuzia kwa Yesu. Alifanyaje hilo? Unawezaje kumpumzika tena wakati kunapokuwa na maafa mengi yanayohitaji umwekee ngao mtoto?

Jibu lilikuwa ni rahisi: Mwamaini Yesu!

“Kila mara unapomweka mtoto wako chini ili alale, mweke kwenye mikono ya Mungu, ambaye huwa halali wa hasinzii” ulikuwa ndio ushauri. “Mpeleke kwa Bwana kwa njia ya maombi na umwache pale.”

Wasi wasi wangu kuhusu SIDS haukumfanya mwanangu kuwa salama zaidi kila usiku. Ulinipa mimi hisia ya bandia ya “kufanya kitu fulani” kwa ajili ya hitaji langu kwani nilikuwa natumia nguvu nyingi juu ya jambo hilo. Lakini, ukweli ni kwamba, hofu yangu haikufanya cho chote kumsaidia apumue usiku mzima.

Kwa hiyo Yesu aliuliza, “Ni yupi kwenu ambaye akijisumbua aweza kujiongeza kimo chake hata mkono mmoja?” (Mathayo 6:27). Wasi wasi wako hauwezi kutatua tatizo, hauwezi kuimarisha hali yako. Ni kinyume chake kabisa. Badala ya kuchangia kitu fulani cha thamani katika hali iliyopo, wasi wasi huutia wingu uamuzi wako, ukiuondoa utambuzi wako, na kukufanya ukose uwezo wa kukabili msongo – pasipo kujali ni msongo wa aina gani.

Una wasi wasi kuhusu fedha zako. Una wasi wasi kuhusu elimu yako. Una wasi wasi juu ya watoto wako. Una wasi wasi juu ya ndoa yako. Unawasi wasi juu ya afya yako. una wasi wasi kuhusiana hali ya ulimwengu na madhara ya muda mrefu ya hili janga la COVID-19. Una wasi wasi kuhusu wakati ujao na juu ya wapi kwa kwenda kutoka hapa. Una wasi wasi juu ya kuwa na wasi wasi kupita kiasi. Hii haiishi!

Hiki ndicho Ellen White alichosema:

Tunapobeba mikononi mwetu usimamizi wa mambo tunayotakiwa kuyatumia kutenda, na kutegemea hekima yetu wenyewe kwa ajili ya mafanikio, tunabeba mzungo ambao Mungu hakutupatia, na tunajaribu kuubeba pasipo msaada wake. Tunajitwalia wenyewe wajibu wa Mungu, na hivyo kwa hakika, tunajiweka sisi wenyewe mahali pake. Ni kweli tunaweza kuwa na wasiwasi na kutarajia hatari na hasara, kwani ni hakika kuwa itatukabili. Lakini tunapoamini hakika kwamba Mungu anatupenda na anakusudia kututendea wema, tutaacha kuwa na wasi wasi juu ya wakati ujao. Tutamtumainia Mungu kama mtoto anavyomtumainia mzazi mwenye upendo. Kisha taabu zetu na mateso yetu vitatoweka, kwani mapenzi yetu yamemezwa ndani ya mapenzi ya Mungu.” —Thoughts from the Mount of Blessing, 100, 101 (1896).

Katika ulimwengu wenye dhambi, tunaweza kuwa na hakika kwamba hali zenye changamoto zitainuka. Hekima ya kidunia husema kuwa njia bora ya kujitayarisha kwa ajili ya majanga ni kujielimisha wenyewe kadiri iwezekanavyo – kuonywa mapema ni kujizatiti mapema. Lakini linapokuja suala la kuleta amani katikati ya dhuruba, elimu haina ufanisi. Kujizatiti pekee kwenye ufanisi ni kukuza tumaini lenye kukaa pamoja na Mungu anayeshikilia mikononi mwake chembechembe ndogo kabisa za mada kwa ajili ya maslahi mapana ya ulimwengu wote. Ashukuriwe, kwani bado yuko katika udhibiti!

Mapendekezo ya aya za ziada za kusoma juma hili:

- [*“Peace, Be Still”*](#), (Desire of Ages, ch. 35) by Ellen G. White
- [*“Surrender – The Secret to Perfect Peace & Happiness”*](#) by Gregory L. Jackson

Siku ya 78, Ijumaa, Juni 12, 2020

MASWALI YA KUJIHOJI MOYONI:

Je! umewahi kupambana kiimani katika nyakati za zahama? Umewahi kupambana juu ya namna ya kujifunza kutumaini wakati hali na hisia zinapoelekea kuonesha kuwa hakuna suluhisho bora lililopo kwa ajili yako? Kwa nini usimwombe Mungu akupatie ujasiri zaidi na imani imara zaidi katika ahadi zake?

CHANGAMOTO ZA MOYONI:

Hofu, wasi wasi, msongo, hiyo ni miitikio ya asili tunapokabiliwa na hali ngumu ambazo hazidhibitiki. Fikiria maisha yako, na familia yako. Ni mambo gani yanayokufanya uyaogope? Ni mazingira gani yanayosababisha uwe na hofu? Sasa fungua Biblia yako na ujaribu kutafuta aya na visa vinavyokuahidi amani na nguvu toka kwa Mungu. Zisome, ziandike, zikariri, na uziamini. Je! Kuna jambo lo lote, kwa hakika, ambalo Mungu wetu hawezi kulishughulikia?

USHUHUDA WA SIFA:

- Pastor H.: anasema, “Asante sana kwa maombi yenu! Binamu yangu na mkewe wako vizuri sasa!
- Mtu fulani alitoa kiasi kikubwa cha fedha ili kusaidia Wainjilisti wa Vitabu ulimwenguni kote wakati wa zahama hii. Wainjilisti wa Vitabu wanapata njia mpya na za kiubunifu za kuwafikishia watu vitabu vya kiroho, licha ya mazuo yaliyopo!

MAMBO YA KUOMBEA:

- **Ombea** imani zaidi na ukweli katika Mungu, hasa wakati huu wa zahama.
- **Omba** baraka za Mungu kwa ajili ya washiriki wanaofanya biashara ya Taxi kule Panama City, Mungu awatumie kama vituo vya mvuto vinavyotembea. Nusu ya raia wa Panama wanaishi katika jiji la Panama City.
- **Ombea** programu ijayo ya Uinjilisti wa Vikundi Vidogo katika Unioni ya Magharibi mwa Nigeria chini ya Idara ya Huduma za Wanawake.
- **Ombea** wanafamilia wako wa karibu na wanafamilia wengine. Waombee wale wasiomjua Yesu kama Mwokozi wao binafsi na bado hawajavutwa kwake na kuongoka.

Siku ya 79, Jumamosi, Juni 13, 2020

UPONYAJI WA KIROHO

“Uniponye, Ee Bwana, nami nitaponyeka; uniokoe, nami nitaokoka; kwa maana wewe ndiwe uliye sifa zangu.”– Yeremia 17:14

“Yule aliyepooza, katika Kristo alipata uponyaji wa vyote viwili roho na mwili. Alihitaji afya ya roho kabla hajafurahia uponyaji wa mwili. Kabla ya kuponywa kwa maradhi ya kimwili, Kristo ni lazima alete unafuu katika moyo, na kuitakasa roho kutokana na dhambi. Somo hili halitakiwi kupuuzwa. Wapo maelfu leo wanaoteseka kwa magonjwa ya kimwili, ambao kama yule mwenye ukoma, wanatamani kusikia ujumbe, “Dhambi zako zimesamehewa.” Mzigo wa dhambi, pamoja na machafuko yake na tamaa yake isiyoridhishwa, ni msingi wa maradhi yake. Hawawezi kupata nafuu hadi watakapokuja kwa Mponyaji wa roho. Amani ambayo ni yeye pekee awezaye kutoa itarejeshwa nguvu katika akili na afya katika mwili.” – Ministry of Healing, p. 77

MASWALI YA KUJIHOJI MOYONI:

Mara nyingi tunamwomba Mungu atuponye homa za kimwili, tukishindwa kutambua kuwa hitaji letu kuu ni uponyaji wa kiroho kwanza. Ndio, maradhi ya kimwili, wakati fulani yanaweza kuhisiwa kuwa ni ya uharaka zaidi na huelekea kuwa na maumivu zaidi kuliko dhambi zilizosamehewa maishani mwetu, lakini usifanye kosa, hakuna jambo lililo muhimu kuliko dhambi zetu kuondolewa kutoka ndani yetu. “Kwa kuwa itamfaidia mtu nini kuupata ulimwengu wote (*pamoja na afya ya kimwili*), akipata hasara ya nafsi yake?” (Marko 8:36). Ni jambo gani jepesi kwako, kumwomba Mungu uponyaji wa kimwili, au utakaso kamili wa dhambi zako na nguvu ya kushinda, hasa dhambi zako uzipendazo? Je! Upo tayari kuvumilia ugonjwa wa kimwili, kwa kadiri unavyodumu kuwa safi kiroho? Kwa nini usimwombe Mungu sasa hivi ili akuoneshe hitaji lako la uponyaji wa kiroho leo?

USHUHUDA WA SIFA:

- Mungu ameleta njia kwa baadhi ya Hospitali za Kiadventista kupokea vifaa vilivyohitajika sana vya kujikinga ili kuwatibu wagonjwa wa COVID-19
- Mikutano ya injili ya AWR kwa njia ya mtandao tayari imekwishavuta mamia ya maelfu ya wafuatiliaji!

MAMBO YA KUOMBEA:

- **Ombea** uponyaji wa kiroho kutokana na dhambi, ubinafsi, na kiburi
- **Mwombe** mwanamke (hakujatwa jina) ambaye amekuwa akishambuliwa na mapepo kwa miaka 15.
- **Ombea** kituo kipya cha Kiadventista cha Uponyaji wa Uraibu kule Orlando, Florida, nchini Marekani, kinachosaidia mapambano dhidi ya kusambaa kwa dawa ya kulevya iitwayo opioid. Ombea mamilioni wanaotamani kuachana na uraibu.
- **Ombea** usiku wa mwisho wa mikutano ya Uinjilisti ya AWR kwa njia ya mtandao na wengi wanaojisalimisha kikamilifu kwa Yesu na kwa ukweli mpya waliojifunza.

Siku ya 80, Jumapili, Juni 14, 2020

UPONYAJI WA KIMWILI

“Bwana atamtegemeza alipo mgonjwa kitandani. Katika ugonjwa wake umemtandikia.” – Zaburi 41:3

“ . . . Yesu ni tabibu yule yule mwenye huruma sasa kama alivyokuwa wakati wa huduma yake ya duniani. Ndani yake mna dawa kwa ajili ya kila ugonjwa, zikirejeshwa nguvu kwa ajili ya kila maradhi. Wanafunzi wake katika nyakati hizi, inawapasa kuomba kama wanafunzi wa zamani walivyooomba. Na uponyaji utafuata; kwani, ‘ . . . kule kuomba kwa imani kutamwoko mgonjwa yule.’ Tunayo nguvu ya Roho Mtakatifu, uhakika uliotulia wa imani, ambao unaweza kudai ahadi za Mungu. Ahadi ya Bwana ‘watahika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya’ (Marko 16:18), bado ni ya kutumainiwa sasa kama ilivyokuwa katika siku za wafuasi. Inawasilisha fursa ya watoto wa Mungu, na imani yetu inapasa ishikilie yale yote inayoyakumbatia.” – Ministry of Healing, p. 226

MASWALI YA KUJIHOJI MOYONI:

Mungu ana nguvu ya kuponya kila ugonjwa kwa neno moja. Ameahidi kwamba wote wanaomwamini wataponywa. Iwe hili ninatokea katika maisha haya, au hatimaye kwenye ufufuo, ni juu ya mapenzi yeke na hekima yake kamilifu. Tunatiwa moyo kuomba wagonjwa kwa imani katika Mponyaji Mwenye uwezo wote. Kila mara hatuwasiliani na uwezo wake wa kuponya hadi tunapokuwa tumemaliza kila uwezekano wa kidunia kwanza; na wakati ni muhimu kufanya yote tuwezayo ili kuzuia ugonjwa na kutibu, kila mara inatupasa kwenda kwa Mungu kwanza na kutafuta uongozi wake tunaposhughulika na ugonjwa.

Je! Unaamini katika uwezo wa Mungu wa kuponya? Unatumaini kwamba yeye anajua ni lini wakati bora wa kuponya, na ni lini sio wakati wa kuponya? Je! Upotayari kuyasalimisha maisha katika mikono yake nyakati za afya ili udumu kuwa mwaminifu katika nyakati za ugonjwa? Utaukubali uponyaji wake unapokuja kwa njia ya kubadilisha mtindo wa maisha?

USHUHUDA WA SIFA:

- Kanisa la Waadventista wa Sabato lilikuwa na uwezo wa kuwapata zaidi ya wamisionari 10,600 wanaotumia mtandao ndani ya siku chache tu. Matokeo yake, maudhui ya Kujifunza Biblia (Adventist Bible Study) inafuatiliwa zaidi na kushika nafsi za juu katika orodha ya mambo yanayotafutwa kwenye Google na YouTube
- Kule Filipino, mamia ya vijana wanaomba katika vinkundi vingi vya maombi na minyororo ya maombi kwa njia ya mtandao. Uamsho na miujiza inafanyika!

MAMBO YA KUOMBEA:

- **Ombea** imani zaidi katika nguvu ya Mungu ya uponyaji. Ombea nguvu ya kupokea mtindo wa maisha wenye afya
- **Ombea** shule za Waadventista ulimwenguni kote kwani zimekumbwa anguko lililoletwa na COVID-19 na zinatafuta njia za kiubunifu za kuwa tayari kuendelea kufundisha na kuzifanya shule zao ziendelee baada ya likizo ya kiangazi.
- **Ombea** Gabon Mission kwani wanafanya Kongamano la Biblia mubashara kupitia mitandao ya Facebook na YouTube hadi juni 26. Omba kwamba Mungu aongoze programu hiyo na kugusa mioyo ya wasikilizaji.
- **Omba** kwa ajili ya uponyaji na urejeshwaji wa kiroho wa familia ya dada D. Mume wake anakabiliwa na aina mbaya ya saratani (multiple myeloma) na ni dhaifu katika imani. Watoto wake wameliacha kanisa na kukumbatia mtindo wa maisha usio wa kibiblia. Wazazi wake ni walemavu kwa sababu ya magonjwa

Siku ya 81, Jumatatu, Juni 15, 2020

AKILI YENYE AFYA

“Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.– Warumi 12:2

“Nguvu zote mbili za kimwili na za kiakili, inapasa zifunzwe kwa upendo, ili ziweze kufikia ufanisi wa kiwango cha juu zaidi.” – Counsels on Health, p. 445

MASWALI YA KUJIHOJI MOYONI:

Akili yenye afya hutegemea, kwa kiwango kikubwa, kile ambacho mawazo yako daima yanatafakari, lishe yako, mazoezi, na uhusiano wenye afya. Kuna miunganiko iliyothibitishwa kisayansi kati ya kile unachokula na jinsi lishe yetu inavyoathiri uwezo wetu wa kiakili. Chakula cha mimea, matunda mengi na mboga za majani, miongoni mwa vingi, huathiri afya ya ubongo kwa namna chanya. Pia, kile tunachochagua kutazama kwa macho yetu na masikio yetu, na pia kile tunachokifikiria daima na kukiongelea, kwa sehemu kubwa kina matokeo katika hali yetu ya kiakili kwa sehemu kubwa.

Je” unachagua kufikiri juu ya mambo ya mbinguni, juu ya mada za haki na utakatifu? Je! Ubongo wako unaushughulisha na mambo yanayolenga Neno la Mungu na mapenzi yake? Lishe yako ikoje? Kuna uwezekano wa kuboresha ili uwe na akili yenye afya, iliyo tayari kuingia katika shughuli za kiroho? Ni lini mara ya mwisho ulipokuwa na mazungumzo ya kina na mtu fulani? Kwa nini usimwombe Mungu akuongoze katika mchakato wa kupata afya bora ya kiakili kuanzia leo?

USHUHUDA WA SIFA:

- Katika maeneo mengi masharti ya kufungiwa yameondolewa na watu wapo tayari kurudi kazini tena. Pia idadi ya maambukizi mapya ya COVID-19 imeshuka katika nchi nyingi duniani kote.
- Elden Ramirez (Mwenyekiti wa Konferensi ya Montana), anasema, “Mwezi Machi zaka hazikuwa pale zilipokuwa. Ile hali tuliileta kwa Mungu kwa njia ya maombi. Tulipokea michango minne ambayo ilirekebisha ule mporomoko! Kila mmoja alikuwa anatarajia kuwa Mwezi Aprili zaka zitashuka pia. Hata hivyo, Mwezi Aprili 2020 ulikuwa na kiwango cha juu zaidi cha zaka iliyotolewa katika miaka 10 iliyopita! Mungu anatoa ili kazi yake iendelee!

MAMBO YA KUOMBEA:

- **Ombea** akili yenye afya na uwezo wa kuchagua kutafakari mawazo ya haki.
- **Ombea** utume wa kanisa katika nchi ya DRC. Ukosefu wa usalama kutokana na makundi ya waasi na hali ya jumla ya kisiasa isiyo na utulivu ni mambo yenye athari hasi kwenye utume wa kanisa. Omba Mungu aingilie kati katika giza na uovu na kuleta uamsho mkuu wa uchaji kwa watu wa eneo hili.
- **Ombea** kituo cha mvuto cha Battambang, nchini Cambodia. Kinahusisha sehemu ya mazoezi ya viungo, mgahawa wa vyakula vya mboga, kiwanja cha michezo, nyumba ya ibada, elimu ya afya, elimu ya muziki, na shule ya lugha. Ombea mibaraka ya Mungu katika mbinu hii yenye njia nyingi na mwombe aikuze huduma na kuwaleta watu ambao amekuwa akiandaa mioyo yao
- **Ombea** washiriki wapya waliobatizwa duniani kote, walioyatoa maisha yao kwa Yesu wakati huu wa zahama ya dunia nzima.

Siku ya 82, Jumanne, Juni 16, 2020

KIASI

“Basi nasema, Enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili.” – Wagalatia 5:16

“Ikiwa nguvu ya uchu ulioendekesha ilikuwa na nguvu kwa jamii (ya wanadamu), kiasi kwamba, ili kuivunja, Mwana wa Mungu mwenye uungu, kwa niaba ya mwanadamu, ilimpasa kuvumilia mfungo wa karibu majuma sita, ni kazi iliyoje iliyo mbele ya Mkristo! Bado, hata kama pambano ni kubwa kiasi gani, analoweza kushinda, Kwa msaada wa ile nguvu ya uungu iliyohimili majaribu makali zaidi Shetani awezayo kuyabuni, yeye, pia, anaweza kuwa mshindi kamili katika vita yake na uovu, na mwisho anaweza kuvaa taji ya ushindi katika ufalme wa Mungu.” – Counsels on Diet and Foods, 167.

MASWALI YA KUJIHOJI MOYONI:

Dhambi imekuwa na inaendelea kuyavuruga maisha yetu katika ngazi zote. Dhambi husababisha ukosefu wa uwiano katika maisha yetu na huwaongoza wanadamu kuelekea kwenye misimamo mikali. Katika eneo la lishe na mtindo wa maisha hili huleta matokeo ya matatizo ya kiafya na lina matokeo hasi sio tu kwetu, bali pia kwa wengine. Ni kwa kuwa na mwunganiko kila siku pamoja na RohoMtakatifu, ndipo tunaweza kupata nguvu na uwezo wa kuwa na kiasi katika mabo yote.

Je! Utachagua leo kumwomba Mungu akuwezeshe kuwa na kiasi katika lishe yako, matumizi yako ya muda, mitandao, na mtindo wako mzima wa maisha? Je! Utashikilia neema yake na kutumainia uwezo wake kukupatia ushindi unapoendelea kumtegemea?

USHUHUDA WA SIFA:

- Jay W.: anasema, “Niliomba ombi mahsusi kwamba Mungu afungue fursa kwangu ya muunganiko na majirani zangu wakati wa hili janga, maana kwa kweli siwajui. Mungu alijibu ombi langu na nimeweza kuwa na mwunganiko nao. Ninajua kuwa nao mpango kwa ajili ya wokovu wao!”
- Mwanzoni mwa mwezi Aprili Redio ya Waadventista Ulimwenguni ikishirikiana na Unioni ya Moldova iliendesha mikutano ya injili kwa njia ya mitandao ya Facebook, YouTube, na Zoom. Wachungaji 28 wa makanisa mahalia ya Moldova walianza kuhubiri kupitia mitandao hiyo. Matokeo yake, sasa tunayo majina zaidi ya 25,500 ya watu wanaofuatilia na watu zaidi ya 40 wamejiandikisha kwa ajili ya madarasa ya ubatizo!

MAMBO YA KUOMBEA:

- **Omba** Roho Mtakatifu akukuze kuwa na kiasi katika mambo yote, na hasa katika suala la hamu/uchu wa chakula, mitandao, na kulala usingizi.
- **Ombea** kanisa Kaskazini mwa Uganda. Ujumbe wa Kiadventista unatangazwa kwa njia ya redio, jambo linalochukuliwa na madhehebu mengine kuwa ni shambulio. Omba ili mioyo iyeyushwe na wengi waweze kuupata ukweli!
- **Ombea** huduma kwa ajili ya wasio na makazi katika jiji la St. Louis, Marekani. Waombe wote wanaoshiriki katika huduma hii wajazwe na Roho wakimwakisi Yesu wanapowahudumia watu wasio na makazi.
- **Ombea** janga la COVID-19 lifikie mwisho.

Siku ya 83, Jumatano, Juni 17, 2020

UMUHIMU WA VIUMBE VYA ASILI

“Bwana Mungu akamtwaa huyo mtu, akamweka katika bustani ya Edeni, ailime na kuitunza.”—
Mwanzo 2:15

“Kristo alipenda kuwakusanya watu kumzunguka chini ya anga la rangi ya bluu, kando ya baadhi ya vilima vyenye nyasi, au kwenye ufukwe wa ziwa. Hapa, akiwa amezungukwa na kazi za uumbaji wake mwenyewe, aliweza kuyageuza mawazo yao kutoka kwenye vitu vya kutengenezwa na wanadamu hadi kwenye vitu vya asili. Katika ukuaji na maendeleo ya viumbe vya asili zilifunulia kanuni za ufalme wake. Kadiri watu walivyotakiwa kuinua macho yao kuelekea vilima vya Mungu na kutazama kazi za ajabu za mkono wake, waliweza kujifunza masomo ya thamani ya ukweli wa kimbingu.” – Ministry of Healing, p. 54

MASWALI YA KUJIHOJI MOYONI:

Idadi kubwa ya watu kwa sasa inaishi kwenye majiji na makazi ya miji. Tukiwa tumezungukwa na vitu vilivyotengenezwa na wanadamu, tukivuta hewa iliyochafuliwa, na kabiliwa na kelele za kudumu, ni vigumu kuwa na muda tulivu, muda wa kutafakari pamoja na Mungu na kufurahia kazi zake za ajabu za viumbe vya asili. Hata hivyo, kutumia muda katika mazingira ya asili huburudisha mwili na akili!

Ni muda wako kiasi gani unautumia katika mazingira ya kutengenezwa au ukitazama maudhui ya kidijitali? Ni mara nyingi kiasi gani unatumia muda kufurahia mazingira ya asili yaliyoubwa na Mungu? Kwa nini tangu sasa na kuendelea usifanye kuwa ni jambo la muhimu kuweka ratiba ya muda wa kuwa pamoja na Mungu katika mazingira ya asili na kujifunza kutoka humo masomo ya kiroho?

USHUHUDA WA SIFA:

- Stephen A.: anasema, “Ninamsifu Mungu kwa ajili ya Siku 100 za Maombi. Ibada za kila siku zimenipatia fursa ya kuomba na kijana wangu wa kiume wa miaka 9.”
- Mtu ambaye hakutajwa jina: anasema, “Siku 100 za Maombi zimenipa changamoto ya kutembea na Mungu kwa karibu zaidi, na kwa uaminifu zaidi. Kwa hakika ninapambana na masuala ya aina mbali mbali, lakini naweza kuona kuwa ushindi unawezekana ndani ya Yesu. Asifiwe!

MAMBO YA KUOMBEA:

- **Ombea** tupate macho ya kiroho tuweze kuona masomo ya kiroho katika viumbe vya asili. Omba Mungu akuoneshe njia za kutumia muda zaidi pamoja na yeye katika mazingira ya asili
- **Ombea** wamisionari, watendakazi wa Biblia walio mstari wa mbele, na watangulizi wa utume ulimwenguni (Global Mission) wanaohudumu duniani kote katika baadhi ya maeneo magumu.
- **Ombea** makanisa ambayo kwa muda mrefu yamekuwa hayana ongezeko/ukuaji ili yapate uamsho kwa ajili ya utume.
- **Ombea** uongozi wa Konferensi Kuu unapotafuta njia bora za kusaidia makanisa mahalia duniani kote wakati wa janga hili.

Siku ya 84, Alhamisi, Juni 18, 2020

**MWANZO MPYA!
(Kanuni 8 za Asili za Afya)**

“Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu.” – 1 Wakorintho 6:19,20

“Pasipo ufahamu wa kanuni za afya, hakuna hata mmoja anayefaa kwa ajili ya wajibu wa maisha.” – Ministry of Healing, p. 271

MASWALI YA KUJIHOJI MOYONI:

Mungu anavutiwa sana na ustawi wetu katika mambo yote. Hana shauku tu ya sisi kuwasiliana naye tunapopitia matatizo ya afya, bali pia, yupo tayari kutusaidia kujifunza namna ya kujikinga na masuala mengi ya kiafya ya siku za leo na kuimarisha mfumo wetu wa kinga. Ndio maana ametupatia kanuni rahisi za kudumu. Kanuni hizi ni: **Lishe Bora, Mazoezi ya kila mara, Maji Safi, Mwanga wa Jua, Kiasi, Hewa Safi, Pumziko, na Tumaini kwa Mungu.** (Ufupisho kwa Kiingereza: **NEW START**). Inawezekana kuwa tayari unazifahamu kanuni hizi, lakini, je, unazifanyia kazi? Kwa nini usizishikilie kanuni za Mungu za afya, na kwa msaada ya Roho wake, ujifunze kuzishika zote?

USHUHUDA WA SIFA:

- Bernard O.: anasema, “Tunamsifu Mungu, alitupatia uwezo wa kufanya utume wa injili kule Kitale, Kenya, katikati ya janga hili. Tulikuwa na uwezo wa kuhudumia mji mzima. Biblia nyingi zilisambazwa!
- Mtu ambaye hakutajwa jina: anasema, “Ninataka kumsifu Mungu! Wakati huu wa kufungiwa niliweza kutazama mahubiri kadhaa ya Kiadventista toka ulimwenguni kote kwa njia ya mtandao. Ushuhuda mmoja kwa kweli ulinigusa. Ulitoka kwa mtu aliyekuwa shoga na Mungu akamfungua. Nimekuwa nikipambana na uraibu wa dhambi ya siri kwa muda mrefu, lakini baada ya kusikiliza ushuhuda huu, nilijua kuwa hakuna lisilowezezana kwa Mungu. Niliomba, na kuomba, na Mungu akanipa ushindi! Haleluya!”

MAMBO YA KUOMBEA:

- **Ombea** uhiari na uwezo wa kutimiza kanuni zote za asili za afya katika maisha yako na ya familia yako
- **Ombea** duka la chakula la Kiadventista kule Kingstone, Jamaica, ambalo linajumuisha vyakula mchanyato vya mboga, pamoja na vitabu vya Kikristo na kona ya watoto. Tafadhali mwombe Mungu awalete wateja sahihi, na amwage upendo wake kwao kwa njia ya wafanyakazi waliko pale.
- **Omba** ili Mungu aamshe ndani ya Waadventista wote shauku ya kina katika maandishi ya Ellen G. white.
- **Ombea** upatikanaji wa misaada kwa ajili ya kituo cha kusaidia familia zenye watoto wenye usonji kule Porto Alegre, Brazil (**Usonji** ni tatizo la kihisi linalo athiri uwezo wa watoto wa kuwasiliana na wengine) Kituo hiki kinaendeshwa na watu wanaojitolea kuweka mazingira wazi kwa ajili ya ushirika. Ombea uongozi wa Mungu, na Roho wake uwe pamoja na wanaojitolea kuifikia jamii.